**Maelezo ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Akihitimisha Mjadala wa Wabunge Kuhusu Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026**

**Dodoma, Jumanne, 24 Juni 2025**

---

## I. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, Ninaomba kukushukuru wewe pamoja na wasaidizi wako walioongoza mjadala huu, Mheshimiwa Musa Zungu (Naibu Spika), Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mwenyekiti wa Bunge), Mheshimiwa Deo Mwanyika (Mwenyekiti wa Bunge) na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mwenyekiti wa Bunge).

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninawashukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya uongozi makini wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kwa uchambuzi wao makini, maoni na ushauri walioutoa *kuhusu Tathmini ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2025/26, na Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/26*.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, na hususani wabunge 97 (*vs 137 in 2024*) waliopata nafasi ya kuchangia hoja zilizopo mezani, kwa michango yao mizuri sana. Tumepokea maoni na ushauri uliotolewa. Mwaka huu kwa kiasi kikubwa michango ililenga kuonesha kazi kubwa iliyofanyika na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Tunawashukuru waheshimiwa wabunge kwa kubainisha kwa uwazi

kabisa kazi na mafanikio ya serikali yaliyopatikana kwa kupitia mipango na bajeti walioidhinisha wao.

**4.** ***Mheshimiwa Spika***, ninawashukuru waheshimiwa mawaziri na Naibu Mawaziri kwa michango yao jana kwa jinsi walivyoainisha kazi zilizofanyika na mafanikio yaliyopatikana kupitia sekta zao.

**5.** ***Mheshimiwa Spika***, Ninaomba pia nimpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa Bajeti nzuri sana aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 12 Juni, 2025. Bajeti hii imepokelewa vizuri sana, sio tu na waheshimiwa wabunge, lakini pia wananchi. Kwa mfano, hivi ndivyo baadhi ya vyombo vya habari vilivyoiona Bajeti Kuu ya ya mwaka huu:

- *Nipashe*: Ni bajeti ya kimkakati
- *Daily News*: Competitive, growth budget
- *The Citizen*: Made for Tanzania
- *Mwananchi:* Bejeti ya kimkakati
- *Habari Leo:* Bajeti yakonga mioyo ya wananchi

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sisi wote hapa mbele ni mawaziri na tunafanya kazi kama timu tukitafsiri na kutekeleza maono, maelekezo na miongozo ya Mheshimiwa Rais, pamoja na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango mbalimbali ya serikali tunayopitisha hapa Bungeni. Hata hivyo, ninaamini mawaziri wenzangu watakubaliana nami kumpa pongezi maalum Waziri wa Fedha kwa kuwa yeye ndiye hutangaza kodi, na kwa kodi hizo anabeba lawama kwa niaba ya serikali. Pamoja na yote haya, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba alijitahidi sana kufanya kazi yake vizuri na ndio maana leo hii tunajivunia kukamilika kwa baadhi ya miradi

mikubwa iliyotumia fedha nyingi zilitokana na kodi za watanzania na ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha huyu alizisimamia vizuri.

## II. UFAFANUZI WA BAADHI YA HOJA

**7.** ***Mheshimiwa Spika***, Nitumie nafasi hii kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa mjadala wa Taarifa niliyowasilisha na Bajeti Kuu ya Serikali ndani na hata nje ya Bunge.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya eneo lililojitokeza ni ***tafsiri ya Ukuaji wa Uchumi:*** Baadhi ya wananchi na wachambuzi wamehoji maelezo ya serikali kuhusu afya ya uchumi wetu, hususani tuliposema kwamba uchumi umeendelea kuwa himilivu katikati ya mdororo wa uchumi wa dunia.

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, Duniani afya ya uchumi jumla hupimwa kwa mambo makubwa mawili: ukuaji wa pato la taifa na mfumuko wa bei. Tukishakuwa na hivi vitu viwili tunaangalia sasa ni kwa kiwango gani ukuaji wa pato la taifa unakuwa na athari chanya katika maisha ya watu kwa kuangalia hali za maisha yao, uwepo wa amani, usalama na utulivu, upatikanaji wa huduma muhimu za jamii na ujenzi wa miundombinu ya uchumi, n.k.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** hebu tuangalie tena takwimu tulizowasilisha.

***a) Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi***

| | ***Ukuaji Halisi (%)*** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ***Mwaka/Wastani*** | ***2020*** | ***2021*** | ***2022*** | ***2023*** | ***2024*** |
| 1. Dunia | -2.7 | 6.6 | 3.6 | 3.5 | 3.3 |
| 2. Nchi zilizoendelea | -4.0 | 6.0 | 2.9 | 1.7 | 1.8 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3. Nchi zinazoibukia na zinazoendelea | -1.7 | 7.0 | 4.1 | 4.7 | 4.3 |
| 4. Nchi za Asia zinazoendelea | -0.5 | 7.8 | 4.7 | 6.1 | 5.3 |
| 5. Nchi za SADC | -4.5 | 4.6 | 4.9 | 3.9 | 3.1 |
| 6. Nchi za EAC | -1.0 | 5.3 | 4. | 15.2 | 1.5 |
| ***7. Tanzania*** | ***4.8*** | ***4.9*** | ***4.7*** | ***5.1*** | ***5.5*** |

***b) Mfumuko wa Bei***

| ***Kundi*** | ***Mfumuko wa Bei*** | |
|---|---|---|
| | ***2023*** | ***2024*** |
| 1. Dunia | 6.7 | 5.8 |
| 2. Nchi zilizoendelea | 4.6 | 2.6 |
| 3. Nchi za Asia zinazoendelea | 2.4 | 2.0 |
| 4. Nchi za SADC | 50.3 | 54.6 |
| 5. Nchi za EAC | 15.5 | 23.4 |
| ***6. Tanzania (4.3 in 2022)*** | 3.8 | 3.1 |

Kwa hiyo, ***Mheshimiwa Spika***, tunachozungumzia hapa ni ukweli kwamba kumekuwa na mdororo wa uchumi kidunia. Pamoja na hali hiyo, uchumi wetu umeonesha ustahimilivu wa hali ya juu sana. Katika kipindi cha miaka 20 uchumi wetu umeweza kukua kwa wastani wa wasilimia 6.2.

**11.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kusema hivi hutujivuni wala hatusemi kwamba tumeendelea sana au safari yetu imeisha au ghafla uchumi wetu sasa umekuwa mkubwa kuliko wa Marekani au Ulaya au Asia ya Kusini Mashariki. La hasha. Tunachosema, na ambacho taasisi zote za kifedha duniani (WB, IMF, AfDB, nk.) zinasema, ni kwamba uchumi wetu umeendelea kuwa imara na himilivu katikati ya mdodoro na majanga ya kidunia. Na sababu kubwa ya hali hii ni kwamba uchumi wetu hautegemia sekta moja. Tumefanikiwa sana katika ku-diversify uchumi. Uchumi wetu

unabebwa na sekta nyingi, sio moja, ikiwemo kilimo, *utalii, huduma, viwanda, madini, sekta ya ujenz*i, n.k.

**12.** ***Mheshimiwa Spika***, siku saba tulizokaa hapa tukijadili Bajeti hii tumeonesha kwa sauti na mifano hatua kubwa tuliyopiga katika nyanja mbalimbali katika miaka hii minne. Nilifanya hivyo katika hotuba yangu. Alifanya hivyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika hotuba yake. Waheshimiwa wabunge waliopata nafasi ya kuchangia wamefanya hivyo katika michango yao, wakijikita kwenye yale makubwa yaliyofanyika katika majimbo yao. Na waheshimiwa mawaziri na naibu mawaziri wamefanya hivyo wakati wanachangia jana wakionesha mafanikio makubwa katika sekta zao. Sikusudii katika hatua hii kurudia ambayo yameshasemwa zaidi ya kutoa muhtasari tu na hitimisho.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika siku hizi saba tumeonesha kuwa Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetekeleza wajibu wake katika nyanja zote. Na tukumbushane kidogo tu kuhusu kazi za serikali ili kuwa na vigezo sahihi vya kupima utendaji wake. Serikali ni chombo cha kusimamia mambo makubwa matatu:

i) Ulinzi na usalama
ii) Haki na sheria
iii) Maendeleo
  - Huduma za uchumi (barabara, reli, umeme, etc)
  - Huduma za jamii (elimu, afya, maji, etc)
  - Mazingira wezeshi katika kufanya shughuli za uchumi: uzalishaji, uwekezaji, biashara, kilimo, etc.

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, Tanzania imejijengea heshima katika mambo mengi. Ukiacha heshima tuliyojijengea ya kuongoza mapambano ya

ukombozi katika bara hili la Afrika, sifa kubwa ya Tanzania inatokana na mafanikio yetu katika kutoa huduma za umma. Tunasifikia kwa kutumia fedha zetu kwa ajili ya kuwekeza katika raslimali za kudumu katika amali ya Taifa yenye thamani kuliko zote, yaani watu wake. Tumefanya hivi miaka yote kwa sababu tunatambua kuwa maendeleo ya kweli ya uchumi hayawezekani ikiwa wananchi ni wajinga au wameelemewa na maradhi ambayo wangeweza kuyazuia. Ndio maana serikali hii ya Rais Samia imewekeza katika kutoa elimu bila ada (elimu ya wali hadi kidato cha sita) na katika kipindi cha miaka minne iliyopita tumetumia shilingi 1,308,900,040,500. Ndio maana serikali ya Rais Samia imetumia shilingi 2,760,000,000,000 kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Na ndio maana serikali ya Rais Samia imeamua kutekeleza mpango wa Bima ya Afya kwa wote na katika Bajeti Kuu yam waka tumeanisha maeneo ya kikodi kwa ajili hiyo.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hakuna shaka kwamba katika miaka hii minne ya uongozi wa Rais Samia kazi kubwa imefanyika na mafanikio makubwa yamepatikana. Sasa wale ambao hawaoni naomba niazime maneno ya Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Ali Hassan Mwinyi. Katika hotuba yake ya kulivunja Bunge la Sita aliyoitoa tarehe 28 Julai 1995, baada ya kuwa ameeleza mafanikio ya serikali yake yaliyopatikana katika kipindi cha miaka kumi ya utawala alisema hivi: ***"Waheshimiwa Wabunge, asiyeyaona maendeleo kwa sababu macho ni magonjwa atege masikio asikilize haya tunayoyasema"***! Kwa hiyo Mheshimiwa Spika, baadhi ya watu kukataa kuona maendeleo katika jamii yetu haijaanza leo. Muhimu ni kwamba wananchi walio wengi wanaona na wanaunga mkono kazi inayofanywa na Serikali ya CCM. Tusonge Mbele!

## III. HITIMISHO

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, Maendeleo ni mapambano ambayo hayana mwisho. Maendeleo ni mchakato endelevu. Katika mchakato huu tutapata mafanikio na tutapata matatizo. Katika mchakato huu yapo mambo tutapatia na yapo mambo hatutafanikiwa na tutafanya makosa. Ndivyo imekuwa hivyo na ndivyo ilivyo. Muhimu katika mchakato huu ni kujua tunataka kwenda wapi na namna ya kufika tunapotaka kwenda.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika uongozi wake wa miaka 24, Mwalimu Nyerere alifanya mengi makubwa. Lakini yapo mambo alikosea na akayasahihisha, ikiwemo kufuta vyama vya ushirika na kufuta serikali za mitaa, ambayo baadaye alikuja akayasahihisha. Katika hotuba yake ya mwisho Bungeni wakati anaaga rasmi kama Rais alihitimisha kwa kueleza mafanikio yake makubwa na matatizo aliyokuwa anaacha. Alisema: "kazi kubwa niliyoazimia kuifanya ni kazi ya kujenga taifa lenye umoja kwa msingi wa heshima na usawa wa binadamu. Tunalo taifa moja lenye umoja, ambalo msingi wake ni heshima na usawa wa binadamu. Akaendelea. ***"Mafaniko yetu ni makubwa sana. Na hasa wananchi; watu wetu sasa wanatembea kwa heshima na kujiamini, na wana haki ya kujivunia kuwa watanzania". Pamoja na mafaniko haya Mwalimu Nyerere hakusita wala kuona aibu kueleza matatizo aliyokuwa anayaacha. Alisema hivi: "…..hali ya uchumi wetu bado ni mbaya na itabaki kuwa mbaya kwa muda mrefu (uk.6)'. Akaendelea: "Tunadaiwa madeni makubwa sana na mashirika ya kimataifa. Lazima taifa letu lipambane na tabia za rushwa na magendo zilizojitumbukiza katika kipindi hiki cha matatizo***".

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa hiyo tunapoeleza mafanikio yetu hapa hatufanyi hivyo kwa kujidai au kwa kusema kwamba sisi tu wajuzi sana

wa kuleta maendeleo. Tunafanya hivyo kuonesha juhudi na jitihada ambazo tumezifanya na mafanikio tuliyopata. Waasisi wa taifa hili walifundisha kuwa muhimu sana katika uongozi ni ujasiri wa kubaini makosa yetu na kuyasahihisha na kubaini ya kubaini matatizo na kupambana nayo kwa wakati.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ujasiri huo unahitaji uongozi makini. Hilo lina kiongozi mwenye ujasiri wa kubaini, kutambua, kubeba na kuyaendeleza mema yote yaliyopita na yanayoendelea. Hilo lina kiongozi mwenye ujasiri wa kubaini makosa yaliyofanyika na kuyasahihisha bila aibu wala haya. Kiongozi huyo kwa sasa ni Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ujasiri huo unahitaji chama makini cha siasa chenye uwezo wa kutoa mwelekeo sahihi wa kisera kwa wakati sahihi na unaokidhi mahitaji ya kizazi cha leo na kesho. Chama hicho kwa sasa ni ***Chama Cha Mapinduzi***.

**20.** ***Mheshimiwa Spika***, Niseme nini tena. Twendeni kwa ujasiri majimboni tukawaombe watanzania wachague kiongozi mwenye ujasiri nilioueleza. Kiongozi huyo ni Dkt. Samia Suluhu Hassan na Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Twendeni kwa ujasiri majimboni tukawaombe watanzania wachague chama makini chenye uwezo wa kutoa na kusimamia mwelekeo sahihi wa kisera kwa nchi yetu. Chama hicho ni Chama Cha Mapinduzi!

## IV. SHUKRANI

**21.** ***Mheshimiwa Spika***, Kuitumikia nchi yetu na wananchi wake katika nafasi ya uongozi kama huu tulio nao sisi mawaziri na sisi waheshimiwa wabunge ni heshima ambayo hakuna mtu yeyote anaweza kusema kuwa anastahili. Ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani na heshima aliyonipa ya kutumikia serikali yake kwa nafasi ya

uwaziri. Ni heshima ambayo imeweka alama ya kuduma katika maisha yangu yote. Ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ubungo Jijini Dar es Salaam kwa imani yao na hata kunichagua kuwa mbunge wao. Ni kupitia kura zao ambazo zimenipatia fursa ya kuweza kuonekana na hata viongozi wetu kuniona. Ninawaheshimu na nitawaheshimu daima.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninamtukuza Mungu kwa yote. Tutafanya yote. Lakini hakuna tuliwezalo bila Mungu. Hata kuonekana kwetu na hata viongozi wetu wakatuona na kwa neema yake tu. Sisi sio kwamba ni wajanja sana au tu wajuzi sana. Hapana. Ni kwa neema yake tu. Mhubiri 9:11 inayosema: ***Nikarudi, na kuona chini ya jua, ya kwamba si wenye mbio washindao katika michezo, wala si walio hodari washindao vitani, wala si wenye hekima wapatao chakula, wala si watu wa ufahamu wapatao mali; wala wenye ustadi wapatao upendeleo; lakini wakati na bahati huwapata wote!***

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, ninakushukuru tena kwa fursa uliyonipa ya kuhitimisha hoja yangu.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninaomba Kutoa Hoja!